BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Nne – Tarehe 11 Februari, 2019.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya mwaka 2018/2019.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

55. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 chini ya Ibara ya 105 bado inatambua kuwepo kwa Waziri Kiongozi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Na kwa kuwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kwa mujibu wa marekebisho ya kumi ya Katiba ya mwaka 2010 imefuta

cheo cha Waziri Kiongozi na badala yake kuweka Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais;

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukuwa hatua gani hasa kupitia vikao vya mashirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili Katiba ya Jamhuri ya Muungano ifanyiwe marekebisho na kuondoa mgongano huo baina ya Katiba zetu mbili.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

54. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa kuwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma tokea mwaka 2016/2017 imeshanunua na kuanza kuvitumia vifaa vya kieletroniki kama vile “saver, UPS, KVM, sitch, motor” kwa ajili ya usajili wa taarifa za mali na madeni ya viongozi wa Umma.

(a) Je, vifaa hivyo vimegharimu kiasi gani cha fedha hadi kukamilika na kuanza kufanya kazi.

(b) Je, mfumo huo una uwezo wa kuhifadhi taarifa za watumishi wangapi na una “Guarantee” ya muda gani kutoka Kampuni zilizopewa kazi hiyo.

(c) Kwa kuwa watu waliopangwa kuhakikiwa kwa mwaka 2017/2018 ni 360 ni changamoto gani zilipelekea kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

60. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara ya Maalum za SMZ:

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliahidi kutengenezwa barabara ya Mwera Polisi hadi Fuoni meli saba kwa kiwango cha lami .

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

75. MHESHIMIWA MASOUD ABRAHMAN MASOUD (Jimbo la Bububu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Eneo la pembezoni mwa uwanja wa Maisara lilikuwa likitumika kwa shughuli za kuadhimisha siku tukufu ya kuzaliwa Mtume wetu Muhammad (S.A.W), kuchezwa michezo kadhaa pamoja na watu mbali mbali kulitumia kama eneo la kujipumzisha na kufanya mazoezi. Hivi karibuni eneo lile limetengenezwa katika eneo lililokuwa likitumika kuegesha vyombo vya usafiri “Parking area”.

(a) Je, kwanini hivi sasa watu wanaotaka kutumia maeneo yale ya Maisara huwa wanazuiliwa kuegesha gari zao katika eneo ambalo awali walikuwa wakilitumia kama “parking area”.

(b) Iwapo wananchi hawaruhusiwi kutumia eneo hilo kama eneo la maegesho. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia eneo mbadala wananchi wanaotembelea maeneo ya Maisara upande wa uwanja wa KMKM ili waweze kuegesha gari zao.

(c) Hivi kwanini Serikali inapoamua kufanya mageuzi ya matumizi ya maeneo hufanya maamuzi yake bila ya kuwajulisha wananchi hususan kwa kuwatangazia ili waweze kuepukana na usumbufu wanapotembelea maeneo hayo na kutaka kuegesha gari zao.

Wizara ya Fedha na Mipango:

120. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Jengo la Darajani Chawel Building ujenzi wake umekamilika kwa muda mrefu sasa na Serikali inaendelea kukosa mapato yakiwemo umeme, ufagizi wa taka na leseni.

(a) Je, kwa nini mpaka leo milango ya maduka hawajapewa wafanyabiashara wale waliokuwa wamepangishwa tangu mwanzo.

(b) Je, kuchelewa kuwapa milango wafanyabishara katika eneo hilo Serikali haioni kuwa inakosa mapato mengi.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

1. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda.

Mnamo tarehe 24/07/2018 vyombo vya habari vimenukuu kauli ya Wizara ikisema watajenga kiwanda cha kusindika mwani pamoja na kufanya utafiti wa mazao na masoko ya mwani Zanzibar.

(a) Je, Kiwanda hicho kitajengwa wapi.

(b) Je, lini mradi huo unategemewa kuanza hasa ikizingatiwa imeshawahi kutolewa ahadi ambayo mpaka hivi sasa havijatekelezwa.

(c) Je, wakulima wa mwani wawe na matumaini gani kwa ujio wa kiwanda hicho hasa ukizingatia bei ya zao hilo ipo chini sana.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

31. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimewekwa katika mkataba wa ujenzi wa jengo la ZURA.

(b) Je, tutarajie ni kiasi gani cha ziada cha fedha kitatumika hadi kukamilika kwa ujenzi wake.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

25. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Karibu miaka 12 iliyopita, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Hata hivyo, kwa sababu mbali mbali Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haikuridhia Sheria hiyo hadi hii leo. Kwa kuwa muda ni mrefu, na kwa kuwa wananchi wengi maisha yao yanategemea sana shughuli za uvuvi.

(a) Je, kuna mapendekezo yoyote ya SMZ ya kutaka kufanyiwa marekebisho Sheria hiyo ili iweze kutumika Zanzibar.

(b) Je, Zanzibar inapata mgao wowote wa fedha kutokana na uvuvi wa Bahari Kuu.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

15. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Pamoja na jitihada kubwa za Serikali katika sekta ya barabara, bado barabara zinazojengwa huharibika haraka na hivyo fedha nyengine hutumika kutengeneza upya barabara hizo na Serikali kushindwa kutengeneza barabara nyengine. Miongoni mwa sababu zinazopelekea kuharibika kwa barabara hizo ni uzito mkubwa wa gari zinazopita

ambapo hivi sasa, gari zenye uzito wa hadi tani 30 hupita katika barabara zetu

(a) Je, kwa sasa barabara tunazojenga zinaweza kuchukuwa uzito hadi wa tani ngapi.

(b) Je, kwa sasa Serikali imetoa ruhusa kwa gari kuwa na uzito wa mpaka tani ngapi kutembea barabara hizo.

16. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Ataamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Katika sekta ya Mawasiliano zipo gari za mizigo hupakiwa bila kiasi mpaka kuhatarisha usalama wa gari na raia katika barabara kwa kipimo cha nafasi ya gari bila kuangalia tani ya gari na uwezo wake.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Je, Askari wa usalama wa barabarani wanatumia vigezo gani katika kukamata gari hizo na kuzipeleka kwenye vyombo vya sheria.

(c) Kwa vile ni jambo la makusudi kwa dereva au mmiliki wa gari kupakia bila kiasi na kuhatarisha maisha ya watu, nini adhabu ya kufanya hivyo.

IV. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Ripoti ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya mwaka 2018/2019.

Zanzibar,
11 Februari, 2019.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.